

# HALMASHAURI YA WILAYA YA SONGWE



## TANGAZO LA ZABUNI YA KUWAPATA MAFUNDI WA UJENZI WA MAJENGO MANNE KATIKA HOSPITALI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA SONGWE

TAREHE 15 NOVEMBA 2021

1. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Songwe anawatangazia wananchi wote kuhusu zabuni ya kuwapata Mafundi wa Ujenzi wa majengo manne katika Mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Songwe. Majengo hayo ni:

- (i) WODI YA UPASUAJI - WANAWAKE (SURGICAL FEMALE)
- (ii) WODI YA UPASUAJI - WANAUME (SURGICAL MALE)
- (iii) JENGO LA UPASUAJI (THEATRE)
- (iv) JENGO LA CHUMBA CHA KUHFADHIA MAITI

2. Hivyo mafundi wanatakiwa kuwa na nguvu kazi ya kutosha kuweza kukamilisha kazi kwa wakati. Mwajiri hataongeza muda kwa fundi yoyote atakaechelewa kufikia lengo.

### 3. SIFA ZA MAFUNDI WANAOHITAJIKA

- Ajue kusoma na kuandika kwa lugha ya Kiswahili kwaajili ya mawasiliano ya maandishi.
- Fundi awe na namba ya utambulisho wa mlipa kodi (TIN).
- Fundi awe na uzoefu usiopungua miaka mitatu na anatakiwa kuonesha uzoefu wa kazi aliozowahi kufanya na kuthibitisha kwa barua kutoka kwa mwaajiri. Fundi mwenye cheti cha VETA atapewa kipaumbele.

- Fundi awe tayari kulipwa kulingana na taratibu za malipo ya Kiserikali hivyo ni lazima awe na Akaunti katika Benki inayotambulika hapa nchini kama vile NMB, CRDB nakadhalika.
- Awe tayari kufuata maelekezo ya Mhandisi Msimamizi wa Halmashauri.

**MAMBO YA KUZINGATIA KATIKA ZABUNI HII:**

1. Halmashauri itanunua vifaa vyote vitakavyohitajika.
2. Fundi atapewa vifaa kulingana na kazi anayofanya na atawajibika kisheria kwa matumizi mabaya ya vifaa ambavyo havikukusudiwa katika utekelezaji wa mradi.
3. Fundi atakaebainika kuiba vifaa vya ujenzi atakuwa amejifukuzisha kazi mwenyewe na hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.
4. Fundi atafanya kazi kwa kufuata maelekezo ya Mhandisi wa Halmashauri katika kutekeleza kazi za mradi.
5. Fundi anaruhusiwa kwenda kutembelea eneo la mradi ili kujionea uhalisia wa kazi kabla ya kuleta maombi ya kazi.
6. Maombi ya zabuni yawasilishwe kwa mkono katika bahasha iliyofungwa vizuri yakionesha Jina Kamili la mwombaji wa zabuni, anuani pamoja na namba ya simu kwa:

**MKURUGENZI MTENDAJI,  
HALMASHAURI YA WILAYA YA SONGWE,  
S.L.P 77,  
MKWAJUNI -SONGWE**

4. Mwisho wa kupokea zabuni ni **TAREHE 22 NOVEMBA 2021** saa **8:00 kamili mchana**. Zabuni zote zitafunguliwa hadharani mbele ya Mafundi au wananchi ambao watapenda kuhudhuria katika ufunguzi wa zabuni. Zabuni itakayochelewa kuwasilishwa katika siku ya ufunguzi katika muda uliotajwa haitafunguliwa.



**CPA CECILIA D. KAVISHE**  
**MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA**

MKURUGENZI MTENDAJI W  
SONGWE